BUNDA HIGH SCHOOL

P.O.BOX. 400. BUNDA - MARA

Tel. +255763 636 680, +255 767 580 540, +255 735 070 190 Email, bundahighschool@gmail.com

KUMB.NA.BSS/GF/J. I/2021 TAREHE: 14/12/2020

MZAZI WA MWANAFUNZI ……

S.L.P …….

BUNDA.

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI BUNDA KWA KIDATO CHA KWANZA- 2021

1:0 Ninafurahi kukujulisha kuwa mwanafunzi tajwa amechaguliwa kujiunga na kidato cha **KWANZA** katika shule hii **Januari 2021.**
Shule ya Sekondari Bunda iko umbali wa ***Km 1½*** Mashariki mwa mji mkuu wa Wilaya ya Bunda mkoa wa **MARA** kando kando mwa barabara iendayo Nyamuswa/Ikizu.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe **11/01/2021. Unatakiwa kuripoti shuleni siku za kazi katika ofisi ya Makamu Mkuu wa Shule kwa mapokezi na usajili kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 15/01/2021.**

2:0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:

2:1 SARE YA SHULE:

(a) ***Kwa Wavulana***:
Ni suruali nyeusi zenye marinda mawili na mifuko mitatu; miwili pembeni na mmoja nyuma, pindo la chini liwe na upana wa sm 3 na mzunguko wa sm 18. Mkanda wa ngozi rangi nyeusi usiwe na bakoli(chuma) kubwa au yenye marembo. Shati nyeupe mikono mifupi, tai nyeusi urefu usivuke mkanda wa suruali – upana sm 7½ na iwe na kibanio.

(b) ***Kwa Wasichana:***
Ni sketi nyeusi zenye marinda ya inchi 1½ mkanda wa sketi usizidi inchi 1½ au sm 4. **Sketi ziwe ndefu ziguse visigino**. Shati nyeupe mikono mifupi, tai nyeusi urefu usivuke mkanda wa sketi upana
sm 7½ na iwe na kibanio,

Kwa Wasichana na Wavulana

- Soksi ndefu nyeupe zisiwe na urembo
- Viatu vyeusi vya kamba vyenye kufunika miguu viwe na kisigino kifupi na visipige kelele wakati wa kutembea kwenye sakafu na isiwe raba.
- Sweta rangi nyeusi ya kuvaa wakati wa baridi.

NB: Rangi ya Hijab ifanane na sare ya shule

(c) **Sare ya Michezo**:

- *Kwa wavulana* ni Truck suit nyekundu na T-shirt nyekundu na raba za michezo
- *Kwa wasichana* ni Truck suit nyekundu, T-shirt nyekundu na raba za michezo

(d) **Sare ya kazi**:

- T-shirt'rangi ya machungwa kwa wote.
- Suruali za kaki kwa wavulana na sketi za kaki kwa wasichana.

NB: Kumbuka kushona kitambaa kizito cha suti na sio kitambaa cha sukari sukari. Sare zote ulizoandikiwa unatakiwa kuja nazo siku ya kuripoti, hazitolewi shuleni(zitakaguliwa). Pia Mwanafunzi haruhusiwi kusuka wala kuwa na ndevu.

2:2 Vifaa vya kutumia darasani

- Daftari kubwa *("Counter book quire 2")* 10, kalamu. (Aje navyo)
- Dictionary English to English (Aje nayo)
- Folder File na kamba yake lisiwe la plastiki (Aje nalo)
- Mathematical set (bofa).

3:0 SHERIA, TARATIBU NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII:

3:1 Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya elimu nchini. Hivyo ni muhimu kwako kumkumbusha mwanao ajue umuhimu wa nafasi hii. Ni kweli usiopingika kwamba malezi ya wanafunzi kitaaluma, kiroho na kimwili yanategemea ushirikiano kati ya walimu na wazazi.

Mwisho, unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
(c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
(d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(e) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
(f) Kutunza mali binafsi, ya mtu mwingine na mali ya umma
(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote

3:2 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE:

1. Wizi
2. Uasherati
3. Ubakaji
4. Ulevi wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile; uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k.
5. Kupigana au kupiga au kutukana mwalimu, mfanyakazi au kiranja.
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
7. Kudharau Bendera ya Taifa
8. Kuoa au kuolewa

9. Kuwa mjamzito /kupata mimba
10. Kutoa mimba
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza fujo au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu wengine
12. Kukataa adhabu kwa makusudi uliyopewa na mkuu wa shule, mwalimu au kiranja
13. Mwanafunzi kuwa na **SIMU** ya mkononi shuleni

4:0 MAMBO MENGINE MUHIMU:

- 'Medical Examination Form' ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali.
- Fomu za Maelezo Binafsi ya Mwanafunzi ambayo itajazwa na mwanafunzi husika.
- Fomu ya Mzazi Kukiri kukubaliana na Sheria, Kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule ambayo itajazwa na Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi husika.
- Fomu ya Mkataba wa kuoboresha taaluma kati ya mzazi/mlezi wa mwanafunzi na shule.

NB: Fomu hizi zitakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti.

5:0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu. Tumia nafasi hii muhimu ambayo Taifa limekupa upendeleo maalumu. Ufikapo shuleni jitahidi kusoma kwa bidii.

ZINGATIA SIKU ZOTE: 'NIDHAMU NI USHINDI'

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

***Mwl.* GALIBONA, MM.**
MKUU WA SHULE